Kwa Pamoja Tunaweza

HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA

Hutolewa kila baada ya Miezi Mitatu Julai-Septemba 2016 Toleo Na 001

Ndani

HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA YAPATA SAFU MPYA YA UOGOZI UK.3

TASAF III YAWA MKOMBOZI WILAYANI SENGEREMA UK.6

HABARI KATIKA PICHA UK. 11&12

Sengerema yatekeleza kwa vitendo agizo la Mhe. Rais Dr. John Pombe Magufuli

WANANCHI WA KATA YA CHIFUNFU (KIJIWENI) WAITIKIA WITO WA KUSALIMISHA ZANA HARAMU KWA HIARI KUPITIA AGIZO LA MHE. MKUU WA WILAYA YA SENGEREMA(DC)

TAHARIRI

Karibuni wapenzi wasomaji wa Jarida letu la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema (***Kwa Pamoja Tunaweza***) ambalo hutolewa kila baada ya miezi mitatu.

Dhima ya jarida hili mbali na kuhabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema pia ni nyenzo na daraja la kukuza maarifa kwa Wananchi na chachu ya maendeleo katika Halmashauri yetu kwa ujumla.

Jarida hili hutolewa na ofisi ya:

Mkurugenzi mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya
Sengerema.
S.L.P 175 Sengerema.

Simu: 0282590162
Nukushi: 0282590249

Barua pepe: dedsengerema@ymail.com
dedsengerema@gmail.com
Tovuti: www.sengerema.go.tz

DIRA: (VISION)

"KUWA NA JAMII YENYE MAISHA BORA NA INAYOISHI KWA AMANI NA UTULIVU"

DHAMIRA: (MISSION)

"KUWAJENGEA UWEZO WA KIUCHUMI WAKAZI WA HALMASHAURI NA KUTOA HUDUMA BORA ZA KIJAMII ZINAZOZINGATIA VIPAUMBELE VYA MAHITAJI YAO KWA KUWASHIRIKISHA KUTUMIA VIZURI RASILIMALI ZOTE ZILIZOPO CHINI YA MISINGI YA UTAWALA BORA"

Sengerema yapata Safu mpya ya Uongozi.

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imepata safu mpya ya uongozi kuanzia Mkuu wa Wilaya, KatibuTawala na Mkurugenzi mtendaji (w) Kufuatia mabadiliko hayo mkuu wa wilaya amekuwa Ndg. Emanuel Erick ambaye anachukua nafasi ya Bi. Zainabu Terack baada ya aliye kuwepo awali kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mkuu wa mkoa wa Shinyanga.

Pia Katibu Tawala wa wilaya amekuwa Ndgu. Allan Agustine, baada ya aliyekuwepo uteuzi wake kutenguliwa na kupangiwa majukumu mengine.

Huku Mkurugenzi akiwa Ndg. Magesa Mafuru Boniphace ambaye amechukua nafasi iliyoachwa wazi na Ndgu. Julius Chalya baada ya kuteuliwa kuteuliwa na Mh. Rais kuwa mkuu wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya.

Bw. Magesa Mafulu Boniphace anakuwa Mkurugenzi wa tisa kuiongoza Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Mkurugenzi Mtendaji anayehama Bw Julius Chalya (Kulia) akimkabidhi nyaraka Mkurugenzi mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Bw.Magesa Mafuru Boniphace (kushoto) Katika Hafla fupi ya Makabidhiano iliyofanyika Halmashauri ya wilaya ya Sengerema

Katika hatua ingine Mkurugenzi mteule ameomba ushirikiano kutoka kwa watumishi wote na hasa wakuu wa idara na vitengo akiamini kuwa wao ni sehemu ya menejimenti hivyo atahitaji sana ushauri toka kwao. Akiongeza kwa kusema.

“ ndugu watumishi wenzangu mimi hapa nimeletwa kusimamia shughuli za uendeshaji wa halmashauri kama kiongozi mkuu lakini si kwamba mambo yote nitafanya au kuamua mwenyewe hivyo basi ushauri wenu ni jambo la mhimu sana ili kufikia malengo ya pamoja kama halmashauri kwa ujumla”

Hata hivyo kwa pamoja watumishi walimwahidi ushirikiano wakisema yeye ndio kiongozi wao mkuu hivyo asiwe na mashaka kuhusu ushirikiano hasa kutoka kwa wakuu wa idara.

Huku akiwaasa wananchi kufanya kazi kwa uadilifu na pia kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwani kufanya hivyo ni kosa na si utaratibu kwa mtumishi wa umma, hivyo kila mmoja ni sharti kuzingatia kanuni na taratibu za utimishi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mkurugenzi mteule aliye vaa suti na tie nyekundu akisalimiana na watumishi baada kukabidhiwa ofisi katika ukumbi wa halmashauri.

Sengerema yatekeleza kwa vitendo agizo la Mhe. Rais Dr. John Pombe Magufuli

Sengerema imetekeleza kwa vitendo agizo la Mhe. Rais kwa vitendo baada ya kuanza kutekeleza maagizo yake kwa kuchoma zana haramu za uvuvi, kupitia kwa Mhe. Mkuu wa Wilaya mwl. Emanuel Kipole na kamati nzima ya Ulinzi na Usalama baada ya kutoa siku saba kwa wote wanaohusika au kujihusisha na uvuvi kwa kutumia zana haramu wanasalimisha zana hizo. Aliongeza kwa kusema, “kila mmoja wetu kwa nafasi yake naagiza muwape taarifa wale wote wanao jihusisha na uvuvi haramu kuacha mara moja” na ikitokea mtu anakamatwa baada ya tareje 09/09/2016 ni dhihili kuwa atakuwa amekaidi agizo langu nililota hivyo hatua kali zichukuliwe dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Katika zoezi hilo la uteketezaji wa zana haramu uliofanywa na kamati ya Ulinzi na Usalama wilaya iliyokuwa ukiongozwa na Mkuu wa wilaya mwenyewe imefanikiwa kuteketeza zana haramu za uvuvi zaidi ya miatano zenye thamani zaidi ya Tsh 66 milion, zikiwemo timba na makokolo.

Sambamba na hilo pia afisa Mifugo na Uvuvi alitumia nafasi hiyo kuwaasa wananchi waishio kandikando mwa ziwa victoria kuhakikisha wanafanya shughuli za uvuvi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa,

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sengerema (DC) mhe. Emanuel Kipole akiteketeza zana Haramu za Uvuvi katika kata ya Busisi

ili sote kwa pamoja tuweze kunufaika na rasilimali zitokanazo na ziwa letu pamoja na vizazi vyetu vijavyo.

Ndipo wananchi wa maeneo hayo walipo mwahidi mkuu wa wilaya kuwa watafanya juu chini kuhakikisha wanalinda rasilimali hizo ikiwa ni pamoja na kuanzisha ulinzi shirikishi ili kuhakikisha hakuna mtu au kikundi kinachojishughulisha na uvuvi haramu.

Akijibu alisema,

“Kwanza napenda kuwashukuru kwa utayari wenu na hasa hili la kuanzisha ulinzi shirikishi katika maeneo yenu, japo niwaombe mjitahidi sana kutojichukulia hatua mkononi hivyo nawaagiza wale wote mtao wakamata wanajishughulisha na uvuvi haramu mhakikishe mnawafikisha katika uongozi ikiwa ni pamoja na kuchoma zana hizo haramu kwa uwazi”

Sengerema ni moja kati ya wilaya nane za mkoa wa Mwanza ambayo sehemu yake kubwa imezungukwa na ziwa Victoria hivyo kufanya wakazi wengi waishio katika wilaya ya Sengerema shughuli yao kubwa ya kiuchumi kuwa ni uvuvi. Ingawa pamoja na kuwa shughuli hiyo ndo tegemezi kiuchumi kwa wakazi wengi waishio katika mkoa wa Mwanza bado baadhi yao wamekuwa wakijishughulisha na uvuvi haramu jambo ambalo mhe. Rais amelipiga marufuku na hivyo kuagiza “wakuu wa Wilaya hakikisheni shughuli zote za uvuvi haramu zinakomeshwa mara moja katika maeneo yenu ikiwa ni pamoja na kuwakamata wale wote wanaojishugulisha na uvuvi huo” alipokuwa akiwahutubia wananchi wa maeneo ya Buhongwa mkoani Mwanza.

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema yazindua mpango mkakati baraza laMadiwani

Halmashauri ya Wilaya Sengerema Imezindua baraza la madiwani ambalo litadumu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015-2020. Baraza hilo lenye wajumbe 35 ambapo madiwani wa kuchaguliwa wapo 26, viti maalumu wako 9 na mbunge mmoja. Kuzinduliwa kwa baraza hilo kunafuatia kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwezi octaba mwaka 2015 ambao ulihusisha Rais, wabunge pamoja na madiwani.

Kuzinduliwa kwa baraza hilo kulikwenda sambamba na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri, Makamu mwenyekiti pamoja na wajumbe wa kamati mbalimbali za kudumu.

Katika uchaguzi huo wa mwenyekiti wa Halmashauri na mwenyekiti wa kamati ya fedha, uongozi na Mipango, ikienda kwa Yanga Makaga ambaye ni diwani wa Kata ya Nyamatongo.

Huku nafasi ya Makamu mwenyekiti wa Halmashauri na mwenyekiti wa kamati ya kudhibiti Ukimwi ikienda kwa Sylivanus Bulapilo.

Na kwa upande wa kamati za kudumu ambazo huduma kwa kipindi cha mwaka mmoja, Salehe Msabaha alichaguliwa kuongeza kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.

George Kazungu alichaguliwa kuongoza kamati ya Elimu, Afya na Maji.

Sambamaba na uchaguzi huo pia madiwani walikula kiapo kilichotolewa na hakimu wa Wilaya huku kikishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa wilaya ya Sengerema, ikiwa ni pamoja na ujazaji wa tamko la viongozi wa umma kuhusu mali na madeni.

Huku wakiahidi kutoa huduma bora kwa wananchi ili kukidhi mataajia yao na serikali kwa ujumla jambo ambalo siku za hapo nyuma ilionekana maadili kushuka na hivyo viongozi kujiona miungu mtu na si wawakilishi wao.

Madiwani wa Halmshauri ya wilaya ya Sengerema wakiwa katika kikao cha baraza la madiwani baada ya kuzinduliwa kwa baraza hilo.

Madiwani watakiwa kuwatumikia wananchi

Mkuu wa Wilaya Mhe. Emanuel Kipole amewataka Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kujikita katika kuwatumikia wananchi ili kukizi matarajio ya wananchi juu ya serikali yao ya awamu ya tano.

Aliyasema hayo katika kikao cha baraza, wakati wa kuhitimisha baraza hilo lengo likiwa ni kuwataka kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia kanunu na taratibu zilizowekwa.

Akizizungumza wakati wa kikao icho Mhe. Mkuu wa Wilaya aliwataka madiwani wote waliochaguliwa kujikita zaidi katika kutatua kero za jamii ikiwa ni pamoja na usimamizi wa mapato na rasilimali za jamii na taifa kwa ujumla.

“Matarajio ya wananchi kwa serikali ya awamu ya tano ni makubwa sana, sana, wananchi watatupima kwa namna tutakavyokidhi kiu na matarajio yao naomba mkajikite katika kuwatumikia wananchi”.

Alisema Bw. Kipole naamini kuwa baraza hili linawatu makini na mahili ambao wataiwezesha Halmashuri yetu ya Sengerema kupata maendeleo kwa kasi zaidi, na kwa sababu ninyi ni wawakilishi wa wananchi basi mkishirikiana vizuri na wataalamu ni dhahili kuwa Halmashauri yetu itapiga hatua kubwa”. Aliongeza Bwn. Kipole.

Pamaoja na mambo yote hayo mhe. Mkuu wa wilaya alitumia fursa hiyo kuwaomba waalamu pamoja na wahe. Madiwani kuwa kitu kimoja katika ukusanyaji wa mapato kwani kwa pamoja ni dhahili kuwa halmashauri itakusanya mapato yake kama inavyopaswa na sisi kama madiwani tusiwe wa kwanza kuwakwamisha wataalamu kufanya kazi yao ya ukusanyaji mapato kwani kufanya hivyo ni kuisababishia halmashauri yetu kuwa katika wakati mgumu kiuendeshaji.

Halmashauri ya sengerema inajumla ya Wahe. Madiwani 34 ikiwa wa kuchaguliwa na wanchi ni 26, viti maalumu ni 09 pamoja na Mhe. Mbunge.

TASAF III YAWA MKOMBOZI WILAYANI SENGEREMA

Wnanchi waishio katika vijiji vya Nyakasungwa, Kamisa, Igwanzunzu pamoja na Itumbili kata ya Nyakalilo wameipongeza serikali kwa kuwasaidia kuboresha hali zao kiuchumi kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini. Ambapo kupitia mpango huo sasa walengwa wameweza kupeleka watoto shule kwani wamefanikiwa kupata mahitaji mhimu ya watoto kama sare za shule, madaftari, viatu, karamu na hata lishe nyumbani imeimarika

Wananchi wa vijiji hivyo wameyasema hayo kwa mkuu wa Wilaya ya Sengerema Ndg. Emanuel Kipole alipokuwa amefanya ziara katika vijiji hivyo ilikujionea pesa zinazotolewa kwa minajili ya walengwa zinawafikia kama seikali ilivyokusudiwa pia kusikiliza changamoto zinawapata katika malipo. Ambapo walengwa walisema changamoto yao kubwa ni uchelewaji wa pesa katika vituo vya malipo, akijibu hoja hiyo mkuu wa wilaya alisema tatizo hilo ni kweli lipo na analifanyia kazi, huku akiwataka wanufaika wote kuhakikisha wanatumia fedha hizo wanazozipata japo ni kidogo lakini wahakikishe wanajishughulisha katika biashara ndogo ndogo lengo ikiwa ni

Mkuu wa Wilaya Sengerema Mhe. Mwl Emanuel Kipole, aliye vaa suti Nyeusi akiongea na walengwa kutoka kata ya Nyakasungwa

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sengerema azindua mradi wa Kituo cha Afya Kamanga

Kutoka kushoto wa pili ni Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sengerema (Mwl. Emanuel Kipole), wa tatu ni Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri (Mr. Yanga Makaga), wanaofuata ni Wahisani kutoka CEDAR Foundation, anayefuata ni Afisa Usafi na Mazingira (W) (Ndgu. Salim Ally) na mwisho ni Wahe. Madiwani wakiongozwa na (Mhe. George) wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kamanga

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mwl. Emanuel Kipole amezindua mradi mkubwa wa ujenzi wa Kituo cha Afya katika kijiji cha Kamanga wenye thamani ya zaidi ya Tsh. Billion 1 katika kata ya Nyamatongo, ambao unatekelezwa chini ya wahisani kutoka CEDAR Foundation. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Mkuu wa Wilaya amesema anayofuraha kubwa juu ya uzinduzu huu wa mradi wa kituo cha afya kwani kwake imekuwa ni “nyota ya asubuhi” kwani ni mda mfupi sana toka achaguliwe kuona miradi hii mikubwa ikitekelezwa katika maeneo yake ya utawala.

Hata hivyo ametoa pongezi zake nyingi kwa wahisani hao kutoka CEDAR Foundation na hasa safu nzima kwa kukubali kufanya kazi katika maeneo yetu.

Pia amewataka wananchi wa maeneo hayo mradi unapo jengwa kuacha tabia ya udokozi wa vitu vya ujenzi mfano cement, misumari, mapati, kwani kwa kufanya hivyo mradi huu utachelewa kukamilika lakini pia utaleta taswira mbaya kwa jamii yote na kuonekana hamna shukrani. Huku akiwaasa wananchi kutumia fursa hiyo ya ujenzi wa mradi,

huo katika maeneo yao kujipatia kipato kwa kufanya shughuli mbalimbali katika mradi huo hasa vibarua na wapishi, huku akimwonya mkandarasi kuhakikisha shughuli zote zinazoweza kufanywa na wakazi wa maeneo hayo ya mradi zinafanywa na wananchi wa maeneo hayo.

Na mwisho amemshukuru Mkurugenzi mkuu wa CEDAR Foundation Mr. Mark O’ Sulvin kwa kukubali kufanya kazi na serikali ya Tanzania hasa katika kutatua kero na shida za wananchi hasa wakina mama wajawazito ambao wamekuwa ni waathirika wakubwa, hivyo ni imani yake kuwa kituo hiki cha afya kitapokwisha tatizo hili litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa au kuisha kabisa.

SHUKRANI

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

Marehemu Alphonce Misanana

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya sengerema anatoa shukrani zake za dhati kawa watu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kumstiri ndugu yetu Mr. Alphoce Misanana.

Ambaye aliyekuwa ni mtumishi katika halmashauri yetu hapa makao makuu ya halmashauri.

Kwa niaba ya uongozi wote wa Halmashauri, pia tunapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote walioshirikiana na ofisi ya Mkurugenzi kumstiri ndugu yetu.

"Bwana alitoa na bwana ametwaa jina la Bwana libarikiwe"
AMINA.

Imetolewa:

Mkurugenzi Mtendaji (w)
Ofisi ya Tehama na Uhusiano
SENGEREMA.

MAKALA
"USAFI NA MAZINGIRA"

WITO WATOLEWA KWA WANANCHI KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA USAFI WA MAZINGIRA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imeeendelea kutekeleza agizo la serikali la kuhakikisha kuwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo yao ya makazi, biashara na taasisi. Kabla ya agizo hilo la serikali utaratibu uliokuwepo awali kuanzia mwaka 2012 ulikuwa ukiwataka wananchi wote kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika Mji wa Sengerema kila siku ya Alhamisi ya mwisho wa mwezi. Wito huo umetolewa na Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Ndugu Ally Salim wakati akielezea mikakati mbali mbali iliyopangwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema katika kuhakikisha kuwa hali ya usafi wa Mji usafi inaendelea kuboreshwa kwa kutumia mikakati mbali mbali ikiwemo;

-Kuwashirikisha viongozi Wakuu ngazi ya Wilaya, Wakuu wa Idara na Vitengo, viongozi wa Kata, vijiji, vitongoji, taasisi mbali mbali, jumuiya za wafanyabiashara pamoja na wananchi wote kwa ujumla kuhakikisha kuwa masuala ya usafi wa Mazingira yanasimamiwa na kutekelezwa kikamilifu kwa kutumia kauli mbiu ***`Uchafu sasa basi, Sengerema iliyo safi inawezekana`.***

-Kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi, biashara na taasisi kwa kushirikisha kikosi kazi maalum kilichoundwa na Watendaji wa Kata pamoja na Maafisa Afya waliopo katika maeneo ya Kata.

-Kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo na kinatumika ipasavyo.

Kutoa elimu ya Usafi wa Mazingira kupitia vyombo vya habari ikiwemo Radio Sengerema.

-Kuhamasisha shughuli za usafi kwa kutumia mikutano ya hadhara katika Kata, Vijiji na Vitongoji.

-Kuanzisha Tozo/Ada ya Usafi wa Mazingira katika maeneo ya Kaya, biashara na taasisi kwa ajili ya kuwafanya wananchi wote kuwajibika kulipia huduma ya uzoaji taka wanazozalisha katika maeneo yao.

-Kuhakikisha maeneo ya biashara yanakuwa na vifaa maalum vya kubebea/kukusanyia taka zinazozalishwa katika maeneo hayo.

-Utekelezaji na usimamizi wa sheria mbali mbali za Kisekta mfano Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2010, Sheria ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Sengerema ya mwaka 2012. Utekelezaji na Usimamizi wa sheria hizi kwa ujumla wake umekuwa wa manufaa kwa vile hatua zimeendelea kuchukuliwa kwa wale wanaokwenda kinyume na taratibu za usafi pamoja na kuhifadhi Mazingira.

WANANCHI WAHAMASISHWA KULINDA NA KUHIFADHI VYANZO VYA MAJI

Ziwa Viktoria ni chanzo muhimu kwa ajili ya kusaidia kupatikana kwa maji yanayotumika kwa shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii zikiwemo kama uvuvi na ufugaji. Aidha kuna vyanzo vingine vya asili katika maeneo mbali mbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema vikiwemo visima, chemi chemi pamoja na malambo yaliyojengwa katika maeneo mbali mbali. Kupitia kamati za Mazingira za Vijiji, wananchi wameendelea kupewa elimu kuhusu kuhifadhi mazingira ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha uendelevu wake unakuwa wa manufaa kwa jamii.

Pia kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Viktoria- Awamu ya Pili **(LVEMP-II)**, Halmashauri ya Wilaya imetekeleza miradi ya uhifadhi wa Mazingira kwa jamii zilizopo pembeni ya Ziwa kwa kutoa elimu na, pia kusaidia miradi midogo iliyo rafiki kwa mazingira kama vile ufugaji nyuki kwa ajili ya kuinua kipato cha wananchi hao ili kupunguza umaskini na hatimaye kupunguza uharibifu wa mazingira. Shughuli za uvuvi unaozingatia hifadhi ya Mazingira pamoja na uopoaji wa Gugumaji ni sehemu ya mradi huo. Jumla ya Kata tano za Buyagu, Katunguru, Nyakaliro, Nyakasungwa na Nyamatongo na vijiji vitano katika Kata hizo zimeshiriki katika utekelezaji wa mradi huo kwa kufanya shughuli mbali mbali za uhifadhi wa mazingira kando ya ziwa.

Jamii yapata Elimu juu ya Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabia nchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

Wito umetolewa kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari katika kukabiliana na athari za mabadaliko ya tabianchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Ili kuweka uelewa wa wananchi vizuri, mradi wa majaribio wa teknolojia ya Biogesi umefanyika katika Kata ya Nyampande na umewavutia wananchi wengi ambao wana mifugo nyumbani ila hawajapata elimu ya kutosha kuhusiana na ujengaji wa mitambo ya biogesi katika makazi yao. Walengwa wa mradi huu ni wakulima na wafugaji ingawa hutegemeana na upatikanaji wa fedha, mradi unaweza baadaye kujitanua katika maeno mengine. Lengo la mpango huu ni kuinua ustahimilivu na uelewa wa jamii kuweza kukabiliana na athari mabadiliko ya tabia nchi **(Raising local communities resilience and adaptive capacity to climate change impacts).**

Hivyo ni imani yetu kuwa ikiwa kila mmnoja atazingatia haya basi usafi na mazingira ya mji wetu yatakuwa bora na mahala pazuri kwa makazi kwa kizazi hiki na vizazi vyetu vijavyo.

MWENGE WA UHURU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA AGOSTI 7, 2016



KUTOKA KUSHOTO NI MAAFISA WA SEIKALI WAKISHANGILIA MWENGE WA UHURU KWA MADAHA KATIKA ENEO LA KAMANGA WAKISINDIKIZWA NA VIJANA KUTOKA JESHI LA MGAMBO, SKAUT PAMOJA NA JESHI LA POLISI

PICHA YA KWANZA HAPO JUU WALIOVAA SKAFU KUANZIA KUSHOTO NI MKURUGENZI MTENDAJI NDG. MAFURU MAGESA PAMOJA NA MKUU WA WILAYA YA SENGEREMA MWL. EMMANUEL KIPOLE, PICHA YA PILI NI MWENGE WA UHURU UKIVUSHWA KUELEKEA NYAMAGANA TAYARI KWA MAKABIDHIANO NA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA NA PICHA YA TATU HAPA CHINI NI UFUNGUZI WA JIWE LA MSINGI KATIKA CHUO CHA UFUNDI VETA ISUNGANG'HOLO

MAMBO YA MKESHA WA MWENGE KATIKA VIWANJA VYA SHULE YA MSINGI SENGEREMA

PICHA YA KWANZA HAPO JUU NI UMATI MKUBWA WA WANCHI WALIOKUJA KUSHIRIKA KATIKA MKESHA WA MWENGE WA UHURU, YA PILI NI KIKUNDI CHA NGOMA KIKITUMBUIZA KATIKA MKESHA NAYA CHINI UPANDE WA KUSHOTO NI MHE. MKUU WA WILAYA YA SENGEREMA NDG. EMANUEL E. KIPOLE WA KATIKATI NI MKIMBIZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDG. JACKSON NA ANAYEFATA NI MHE. MBUNGE WA JIMBO LA SENGEREMA NDG. WILLIAM NGEREJA NA KULIA NI JESHI LA MGAMBO.